JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

## VWAWA SEKONDARI

**Juni, 2023**

**Dodoma**



CS CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**

**YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu**

Mkuu wa Shule -**0755 535 637**

Makamu Mkuu wa Shule-**0753 707 894**

Matron/Patron - **0769961877**

Shule ya Sekondari -**VWAWA**

**S.L.P. 224 MBOZI-SONGWE**


Tarehe JUNE 2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**………………………………………………. S.L.P**

**………………………………………..**

**……………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI VWAWA HALMASHAURI YA MBOZI MKOA SONGWE MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **Vwawa** ipo umbali wa Kilometa 0.5 km Kusini-Magharibi mwa Mji wa **Vwawa**, Usafiri wa pikipiki/bajaji kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Vwawa. Nauli ni Shilingi 1000/= kwa pikipiki na Shilingi 1000/= kwa bajaji, pia unaweza tembea kwa mguu kufika shule ilipo.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe kuanzia tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30/09/2023**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**



CamScanner

i. Sare ya shule sketi mbili za malinda moja ya rangi ya machungwa (orange) na nyingine rangi ya zabibu (blue violet) zinazofika kwenye kisigino (ndefu). ii. Mashati meupe mawili(2) ya mikono mirefu na sweta rangi ya damu ya mzee (Maruni)

iii. Viatu vyeusi pea moja visivyo na kisigino kirefu na Raba nyeupe pea moja (isiyo na mchanganyiko wa rangi yoyote) ya kamba isiyo na kisigino kirefu) kwa ajili ya kuvaa darasani.

iv. Tai moja (1) ya Orange.

v. Rangi ya Ijabu kwa waislamu ni nyeupe (White) na rangi ya waridi (Pink) kwa muda usio wa darasani.

vi. Nguo za kazi au gauni mbili rangi ya blue mkapa.

vii. Track suit rangi nyeusi isiyobana chini na raba kwa ajili ya michezo. viii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika visipungue viwili (orodha imeambatishwa.

ix. Mashuka pair 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1, foronya 1 na chandarua 1.

x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

**MUHIMU:**
**Mwanafunzi aje na nakala ya hati ya matokeo (result slip) ya kidato cha nne (iv)**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-** I. Ream ya karatasi 2(kwa mwaka).

II. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa).

III. Scientific calculator kwa CBG na EGM na wanao chukua masomo ya Geograpy.

IV. Godoro la futi 3(3 X 6)

V. Mashuka pair 2 rangi ya blue bahari, blanketi 1, foronya 1 na chandarua 1.

VI. Passport size nne (4).

VII. Soksi nyeupe nzito zisizo na maua jozi mbili, kiatu cheusi cha ngozi na cha kamba kisicho na kisigino kirefu na raba nyeupe ya kamba.

VIII. Mavazi mengine ni nguo za ndani za kutosha, taulo, blankenti mbili (2), mashuka mawili (2) rangi ya (blue bahari), bed cover lisilotariziwi maua yoyote, mto, foronya nyeupe, sanduku imara lenye kufuli na chandarua rangi nyeupe au zambalau.

IX. Kijiko cha kulia chakula, sahani na kikombe,

X. Ndoo mbili za lita 10 ya kuogea na kutunzia maji kwa mwanafunzi.

**VIFAA VYA USAFI VINAVYOHITAJIKA SHULENI KULINGANA NA KOMBI HUSIKA:**
Kutokana na uhaba wa vitendea kazi hapa shuleni mwanao aje na vifaa vifuatavyo:

a. CBG- walete na Toilet brush 1 mfagio wa chelewa 1. Mkasi wa kukatia maua , soft bloom 1
b. EGM -walete hard broom 1, mfagio wa chelewa 1, panga 1, mopa na ndoo yake ya kudekia 1,
c. HGK –walete, Kwanja 1, jembe 1, reki 1 mfagio wa chelewa 1
d. HKL - walete Kwanja 1, jembe 1, reki 1 mfagio wa chelewa 1
e. HGL - walete Kwanja 1, jembe 1, reki 1 mfagio wa chelewa 1



CamScanner

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MICHANGO MINGINE YA SHULE**

Michango ya shule mwanafunzi utalipa kwa kupitia akaunti namba **61201000008 NMB** Jina la akaunti ni **VWAWA SECONDARY SCHOOL**.

Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip ya bank. Pindi afikapo shuleni aiwasilishe kwa Mhasibu/mwalimu wa fedha wa shule.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.



CamScanner

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 MAHUDHURIO

**Kila mwanafunzi anatakiwa:**

i. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo.

ii. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa. iii. Kuhudhuria katika kazi za mikono.

iv. Kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa,mikutano ya nyumba na madarasa.

### 3.3 MAANDALIO YA JIONI

**i.** Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 usiku.ispokuwa siku ya Jumamosi ambapo wanafunzi wanaruhusiwa kuangalia TV katika ukumbi wa shule baada ya kipindi cha dini saa 1:30 jioni.

Mwanafunzi haruhusiwi kukaa au kulala bwenini muda huo ukipatikana adhabu itatolewa dhidi yake.

**ii.** Walimu wa zamu watasimamia maandalio ya jioni kikamilifu.

### 3.4 MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:-

- Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mku wa shule.
- Ni kosa kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu:
  - Chumba cha waalimu (Staffroom).
  - Ofisi za shule.
  - Maabara.
  - Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

### 3.5 UGONJWA

**A.** Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, na kwa matroni wa shule. Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa yoyote bwenini. Dawa zote zitunzwe kwa matroni.

**B.** Mwanafunzi mgonjwa ataruhusiwa kupumzika sehemu maalumu kwa kibali cha matron na endapo atazidiwa atapelekwa hospitali.

**C.** Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au Matron wa shule, mara afikapo shuleni.

**D.** Shule haitoi **CHAKULA MAALUMU (Special diet)** kwa mwanafunzi mgonjwa.



CamScanner

**3.6 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi. xix. Kutoka na Kulala nje ya mipaka ya shule bila ruhusa (Utoro).
xx. Kuwasha mshumaa bwenini/kukutwa na kiberiti

**ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI**

1) Mtoto akishapokelewa shuleni, Mzazi/Mlezi au ndugu yeyote harusiwi kuja kumwona labda uitwe na uongozi wa shule au ikitokea sababu isiyozuilika.
2) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu na kifaa chochote cha simu, vyakula vya aina yoyote na mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mtu wa nje ya shule yafanyike tu kupitia uongozi wa Shule.
3) Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa sare ya shule

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANFUNZI**

1) Jina lako kamili lilivyotumika kidato cha nne…………………………………………………………………
Dini/dhehebu……………………………..
2) Jina kamili la Baba Mzazi/Mlezi…………………………………………………
Kazi yake……………………………………………………………………………
Anwani kamaili ya Baba Mzazi/Mlezi…………………………………………
Namba za ya simu ya mkononi………………………………………………… Namba yake ya simu ya mezani…………………………………………………..
Mahali anakoishi Baba Mzazi/Mlez: Mkoa…………........... Wilaya………………
Tarafa…………………….........Kijiji/Mtaa…………………………………………



CS CamScanner

3) Jina kamili la Mama Mzazi/Mlezi…………………………………………………… Kazi yake………………………………………
Anwani kamaili ya Mama Mzazi/Mlezi……………………………………………
Namba za ya simu ya mkononi…………………………………………………… Namba yake ya simu ya mezani…………………………………………………
Mahali anakoishi Mama Mzazi/Mlez: Mkoa……............. Wilaya……………… Tarafa……………………..........Kijiji/Mtaa……………………………………

4) Hapa Songwe nina/sina ndugu
Endapo una ndugu jaza jedwali lifuatalo na bandika picha zao.

**NB: Kila mwanafunzi analazimika kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

1. **Sehemu ya Mwanafunzi**
   Mimi…………………………………………ninakubali nafasi niliyopewa kidato cha tano mwaka……………… Katika shule ya Sekondari **Vwawa** na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kuwa nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea. Anuani yangu ya kudumu Ni…………………………………..
2. **Sehemu ya Mzazi/Mlezi**
   Mimi……………...............................ninakubali mtotowangu……………………………

Kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari Vwawa na nitafika shuleni bila kuchelewa.Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake wa shule na Taifa. Na nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma, tabia na mwenendo wa mtoto wangu nikishirikiana na walimu. Anuani yangu ya kudumu ni………………………………………………………………………………………………………………

Namba ya simu………………………………………………………………………………..
Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandashi.
Sahihi…………………………….. tarehe…………………..

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**



CamScanner

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

VWAWA SECONDARY SCHOOL,

P. O. BOX 224,

MBOZI.

DATE...............

To:

THE MEDICAL OFFICER,

......................................

......................................

Please examine...............................................................................................

As to her fitness for pursuing further education at this school.

1. Haemoglobin..............................................................................

2. P.V.Blooding..............................................................................

3. (A) Blooding.............................................................................. (B) Hearing..............................................................................

4. Blood Pressure..............................................................................

5. Urine for Sugar and Pregnancy tests.....................................

6. Stool for routine examination..................................................

7. Asthma..............................................................................

8. Skin diseases..............................................................................

9. Leprosy..............................................................................

10. Pulmonary tuberculosis..........................................................

11. Employs..............................................................................

12. Deformity..............................................................................

13. Mental problem..............................................................................

14. Comments..............................................................................

..............................................................................................................

.................................

DESIGNATION

**ANGALIZO KWA MWANAFUNZI**

I. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule.

II. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k.

III. Ni kosa mwanafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza Mazingira ya shule

IV. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**MWANAFUNZI ANASHAURIWA KUJA NA VITABU VISIVYOPUNGUA VIWILI (2) VYA MASOMO ANAYOSOMA, VITABU VYA ZIADA (REFERENCES) KAMA IFUATAVYO:-**

A. CHEMISTRY (1&2)

**i.** Chemistry Advanced Chemisrty Review by William W. Davis (Mzumbe book shop project, 2004).

**ii.** Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe book shop project, 1998). **iii.** Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II.(Tanzania instate of education ,1995).

**iv.** Organic Chemistry volume I. The Fundamental Princinples by I.L. Finar (Longman Ltd 1990.

**B. BIOLOGY**

**i.** New Understanding Biology By Suzan Toole.

**ii.** Advanced biology principles and application by C.J. Clegg and D.G. Mackean. **iii.** Advanced biology by Michael Kent.

**iv.** Dissecting Kit. (compulsory ).

**C. ENGLISH**

**i.** Advanced learner's English language for Tanzania secondary school by Abraham Mulungu.

**ii.** Advanced level English by Nicholous Asheri.

**iii.** Advanced level English language 1by shadrack ndambo and James Kinunda.

**D. HISTORY**

**i.** Lesson notes for advanced certificate of secondary education (history paper one and history paper two) by Bakari Madaya.

**ii.** Essential in advanced level history paper 1by salehe Yasin. **iii.** Essential in advanced level history paper 2 by Salehe Yasin. **iv.** Learning advanced African history book one by Idrisa R Msuya.

**v.** Learning advanced World history book two by Idrisa R Msuya.

**vi.** Fundamental principles of history one by Mangoti B. **vii.** Fundamental principles of history two by Mangoti B.

**viii.** Modern world history by Ben Walsh.

**E. ECONOMICS**

**i.** Essentials for economics 1 by Odhiambo Ambrose. **ii.** Essentials for economics 2 by Odhiambo Ambrose. **iii.** Economics for advanced level paper 1 by Ambilikile C.M.

iv. Economics for advanced level paper 2 by Ambilikile C.M

F. **MATHEMATICS**

i. Advanced mathematics for advanced level Book 1&2.
ii. Conceptual advanced mathematics for secondary school's form v&vi. iii. Advanced Mathematics Vol. I and ministry of education and vocational training.
iv. Advanced Mathematics by shayo.
v. Advanced Mathematics by Tranter and Laube. vi. Pure Mathematics vol. I and II by Back House.
vii. Further Pure Mathematics by Bostock and Chandler Rourke.

G. **GEOGRAPHY**

i. J.W.NJIKU , The essential of practical Geography A level.
ii. D.T.MSABILA, An intergrated focal region on Human and Economic Geography-A level.
iii. D.T MSABILA(2019) Comprehensive Approach to Physical Geography A-level.

H. **KISWAHILI**

i. Kiswahili shule za sekondari fasihi kidato cha tano na sita (TET).
ii. Kivuli kinaishi (saida Mohamed).
iii. Mfadhili (Hussein tuwa). iv. Vuta nikuvute (shafi adam shafi).
v. Kunga za fasili na lugha (msokile 1992).
vi. Sarufi ya Kiswahili sekondari sekondari na vyuo (mdee) Dup-Dsm. vii. Historia ya kiswahili Afrika mashariki (Shiragrin na mnyampala).
viii. Tafsiri na ukalimani (mwansoko).

**KARIBU SANA VWAWA SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ......FMagaza......

**Jina la Mkuu wa Shule .FAINES C. MAGWAZA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ............................ THE HEADMISTRESS VWAWA SECONDARY SCHOOL BOX 224-MBOZI

**MHIMU**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo: -**

- **Mkuu wa shule -0755535637/0782218884**
- **Makamu Mkuu wa Shule -0753707894**
- **Mwandamizi Taaluma 0714807633**
- **Mwandamizi Malezi/Nidhamu -0764510888**



CamScanner